Uhuru Uk.1, Julai 9,2021

UhuruDigital, Website uhurum

Rais Samia aanza kuwatajirisha wafugaji, wavuvi

Uk. 2

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega



Scanned with CamScanner

TALIRI kuwainua wafugaji kiuchumi

Na Elizabeth Zaya

TAASISI ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI) imesema imepania kuinua hali ya uchumi ya wafugaji kwa kuwapa mbinu bora za ufugaji.

Akizungumza jana katika Maonyesho ya 45 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam (DITF), Mtafiti Mwandamizi wa Mifugo kutoka taasisi hiyo, Valentino Urasa, alisema ina vituo saba ambavyo pamoja na shughuli yao kuu, imekuwa ikiwaelimisha wafugaji kufuga kwa tija.

Urasa alisema lengo la taasisi yao ni kuona wafugaji wanafuga mifugo iliyo bora na yenye kuleta tija ya kukuza uchumi wao na wa nchi kwa ujumla.

"Taasisi yetu inatoa huduma ya ufugaji katika kanda zao mbalimbali na kila mara tunapita kwa wafugaji kutoa elimu kwa sababu tunataka waachane kabisa na kufuga kizamani bila faida," alisema Urasa.

Mtafiti wa taasisi hiyo, Walter Mangesho, aliwahamasisha wafugaji kuhakikisha wanatumia teknolojia ya matumizi ya malisho bora ili kuhakikisha mifugo inakuwa na afya bora na kuwaletea faida kubwa.

Alisema teknolojia hiyo ya malisho bora kwa mifugo ni kuhakikisha wanaotesha majani ya kisasa yenye virutubisho kwa ajili ya mifugo hiyo.

Nipashe Uk.10, Julai 9,2021

Scanned with CamScanner

Machinjio Vingunguti kuanza kazi Agosti

Na Lucy Lyatuu

MACHINJIO ya kisasa yaliyopo eneo la Vingunguti jijini Dar es Salaam yanatarajiwa kuzinduliwa rasmi Agosti mosi mwaka huu.

Machinjio hayo yanatarajiwa kuwezesha ng'ombe takribani 1,000 ; mbuzi na kondoo zaidi ya 1,000 kuchinjwa kwa siku.

Mradi ulitarajiwa kukamilika Julai mosi, ikiwa ni agizo lililotolewa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa baada ya kutembelea eneo hilo, Mei mwaka huu.

Akizungumza jana katika eneo hilo la machinjio baada ya kufanya ziara, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla aliwaagiza watekelezaji wa ujenzi wa mradi huo kuhakikisha ujenzi huo unakamilika ili uanze kufanya kazi. Mradi huo unagharimu jumla ya Sh bilioni 12.49.

"Mradi huu umekuwa ukisuasua kwa muda mrefu, kila mara wakisogeza muda wa eneo hilo kuanza kutumika, lakini kwa sasa lazima ukamilike na uanze kufanya kazi," alisema Makalla baada ya kuuliza maswali kwa mjenzi wa mradi huo ambaye ni Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) sababu za kucheleweshwa mradi.

Makalla alisema kukamilika kwa mradi huo ni mojawapo ya njia itakayobadilisha maisha ya wananchi kiuchumi kwa kuwa ni wa muhimu wenye kufungua fursa kwa mikoa mingine pia.

Alisema Dar es Salaam inategemewa kwa biashara ya mifugo, hivyo ni vyema kuwa makini na kuanza kwa machinjio hiyo kwani wafanyabiashara watajipanga wakitegemea soko hilo ili kuweza kupanua wigo wa kazi zao.

Awali akitoa taarifa ya mradi huo, Kaimu Mkurugenzi Uendelezaji Biashara kutoka NHC, Margaret Ezekiel aliahidi kuanza rasmi kwa machinjio hayo Agosti na kwamba kilichowacheleweshwa ni uunganishwaji wa chombo cha kuchemshia maji pamoja na tangi la maji.

Aidha alisema walishindwa kuanza rasmi kwa muda alioahidiwa Waziri Mkuu kutokana na ukosefu wa fedha wa kukamilisha mifumo mbalimbali itakayowezesha utendaji kuwa rahisi.

Mkurugenzi wa jiji hilo, Jumanne Shauri alisema ujenzi wa mradi huo umefikia kiwango cha asilimia 96 na kwa sasa wanaendelea kuhakikisha uwepo wa viyoyozi katika eneo la kuchinjia, kujenga eneo la kuhifadhi mbolea na hata eneo la kuwekea utumbo.

Scanned with CamScanner

Ulega aagiza ofisa mifugo kupelekwa kijiji cha wafugaji

Mkuranga
NA SCOLASTICA MSEWA

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amemuagiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga kumhamisha kituo cha kazi ofisa mifugo Kata ya Vikindu kupelekwa katika eneo lenye shughuli za ufugaji.

Ulega aliyasema hayo juzi wakati akikagua maendeleo ya ujenzi wa daraja linalounganisha Kata ya Vianzi na Kata ya Shungubweni, Mkuranga mkoani Pwani.

Naibu waziri huyo ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo la Mkuranga (CCM), alisema ofisa mifugo huyo anapaswa kupelekwa katika maeneo yenye shughuli za mifugo na siyo yenye viwanda.

"Kata ya Vikindu ni eneo la viwanda tena viwanda vya chuma, sio sahihi kuweka ofisa mifugo ambaye hana kazi yeyote hapa wakati kuna maeneo yenye mifugo ambayo hayana wataalamu wa mifugo.

"Nimemwambia mkurugenzi amwamishe ndani ya wiki, ampangie katika vijiji vyenye wafugaji na migogoro mingi ya wafugaji, kwa sababu moja ya sababu za migogoro ya wafugaji ni ukosefu wa wataalamu mifugo watakaotoa ushauri kwa wakulima na wafugaji,"alisema.

Ulega alisema ukosefu wa wataalamu wa mifugo ni miongoni mwa sababu za migogoro vijijini, kwani hakuna wa kuwashauri wakulima na wafugaji kufanya shughuli zao kitaalamu.

"Nataka apangiwe katika kijiji chenye mifugo na ninataka nikamuone katika kijiji hicho akifanyakazi kuwasaidia wafugaji na sio kukaa katika kata ambayo hakuna wafugaji," alisema.

Askari wanaodaiwa kuuza dawa za kulevya Pemba kikaangoni

Pemba
NA MASANJA MABULA

MKUU wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, Salama Mbarouk Khatib, amemuagiza Kamanda wa Kikosi Maalumu cha Kuzuia Magendo (KMKM) Kamandi ya Pemba kufuatilia na kuwasilisha taarifa ofisini kwake kuhusu uwepo wa askari wa kikosi hicho wanaodaiwa kuhusika na biashara haramu ya dawa za kulevya.

Salama alitoa agizo hilo

Scanned with CamScanner

Rais Samia aanza kuwatajirisha wafugaji, wavuvi

Dodoma
BAKARI MNKONDO NA MUSSA YUSUPH

SERIKALI ya Awamu ya Sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan imeanza kutekeleza mipango itakayowatajirisha wananchi wake katika sekta ya mifugo na uvuvi.

Kutoka kutimiza azma hiyo, imeanza utekelezaji wa mpango wa uhuru wa kumarisha uchumi wa bluu kwa kununua meli nane za uvuvi, programu ya unenepeshaji mifugo kwa kuhamia nyasi za kisasa zenye virutubisho, ufugaji samaki na jongoo bahari.

Aidha, serikali imeanza utafiti wa kuku wa kienyeji aina ya kuchi kwa lengo la kufanya Tanzania kuwa nakuku wa kipekee watakaokuwa na uwezo wa kustahimili magonjwa.

Akifungua na gazeti hili kuhusu mafanikio ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, katika kipindi cha siku 100 tangu Rais Samia aingie madarakani, Naibu waziri wa wizara hiyo, Abdallah Ulega, alisema katika siku hizo 100, Rais Samia ameonyesha uthubutu, utayari na uhodari wa hali ya juu kufanya sekta ya mifugo na uvuvi kuwa ya kibiashara.

MIFUGO

Ulega alisema katika kumarisha sekta ya mifugo, Rais Samia mara kadhaa amekuwa akisisitiza kupitia mikutano yake na hata alipolihutubia Bunge alieleza kwamba anataka kuona wafugaji wa kisasa na siyo kuona ng'ombe na mchungaji wakikonda.

Alisema katika kufanikisha hilo, serikali imeendelea kutekeleza programu ya unenepeshaji mifugo, nia ikiwa ni kuhakikisha nyama inayozalishwa nchini iwe na soko la uhakika nje ya Tanzania.

"Rais Samia hakuishia kusema, alimpokea mwana mfalme kutoka Saudia na kubwa lilikuwa biashara ya mifugo. Saudia wanachukua mifugo mingi katika sikukuu ya Eid al Haji, wanachinja idadi kubwa ya mbuzi," alisema.

Ulega aliongeza kuwa: "Lazima tujue kwamba mifugo ilyopo iwanue Watanzania kupitia biashara. Hii ni wizara ya biashara na ndiyo mana (Rais Samia) amekuja kutuonyesha kwamba hiyo ni wizara ya biashara kwa hiyo tufuge kisasa, tunenepeshe, tuuze ili tumarike kiushumi."

KODI ZILIZOONGOLEWA

Ulega alisema ndani ya siku 100 za uongozi wa Rais Samia, ameondoa kodi kwa baadhi ya maeneo ambayo yalikuwa yakiumiza wakuaji wa sekta ya mifugo.

Alisema miongoni mwa kodi ilyoondolewa ni katika kusafirisha nyama, ambapo awali ilikuwa ikilipwa kwa kilo, hivyo kutotabirika bei ya nyama kutoka Tanzania kuwa juu, lakini sasa tatozwa kwa idadi kupitia kibali maalumu.

"Tunahitaji kusafirisha zaidi nyama za mifugo ili tupate fedha za kigeni na kukuza uchumi kutoka kutusia," alisema.

Pia alisema kodi nyingine ilyopunguzwa ni ya vifaa maalumu vya kuzunguka maziwa ambayo awali ilikuwa ikutobolsha vifaa hivyo kuuzwa kwa bei ghali.

"Kutoka dhana, maziwa hayatakiwi kubebwa kwenye chombo chochote ni kinyume cha utaratibu na ndiyo maana kuna vyombo maalum vya aluminiamu vya kubebea maziwa ambavyo sasa kodi imepunguzwa.

"Tunategemea baada ya hatua hiyo, itavutia zaidi watu kuwekeza nchini badala ya kuagiza kutoka nje ya nchi na tutaziishia wenyewe," alisema.

Naibu waziri huyo alisema Tanzania ina uhakika wa kuzalisha maziwa wastani wa zaidi ya lita bilioni 2.5 hadi bilioni tatu kwa mwaka, lakini maziwa mengi yanaharibiwa hususan maeneo ya vijijini kwa kukosa vifaa vya kuhifadhia.

"Mfugaji yupo kijijini, amekusanya ng'ombe wake wa kienyeji ambao kwa wastani wanatoa lita moja hadi tatu kwa siku. Kama ana ng'ombe 10 atapa lita 10 ya maziwa ambayo yapo atakayotumia kwa ajili ya familia, lakini mengine yatabaki.

Alieleza kuwa "Kwa sababu yupo maeneo ya vijijini na hakuna vyombo vya kuhifadhia na maziwa yanatakiwa kufikishwa katika kituo cha kukusanya yakiwa na ubora mfugaji atalazimika kuyamwaga."

Alisema endapo vifaa vya kutunza maziwa vitapatikana kwa wingi na bei rahisi, wana kiji watahifadhi maziwa yao tehemu salama na hatimaye kupata soko la uhakika badala ya kuyamwaga.

KOPA NG'OMBE LIPA NG'OMBE

Ulega ambaye ni Mbunge wa Mkuranga (CCM) alisema wizara hiyo kwa kushirikiana na Benki ya Kilimo Tanzania (TADB) imeanyesha dhamira ya kutoa sh. bilioni 20.

Alisema mradi huo utahusisha kukopesha vikundi vya wafugaji wanaeno kwa ya vijijini Tanzania Bara na Zanzibar kwa kuwapatia mkopo ya ng'ombe na mbuzi ambayo watatakiwa kuanyesha baada ya mifugo hiyo kuzaa.

"Tunasema tuna mifugo mingi, lakini kama akija mtu atakaa tuni 100 za nyama kila mwezi upatikanaji wake ni shughuli. Tunatengeneza mfumo ambao utunusha uwezo wa utambazaji na mahitaji kwa kuwekutanisha wafugaji na wahitaji wa nyama kwanzabuu wamunuzi wa nyama wanahitaji upatikanaji nyama wa uhakika," alieleza.

Aidha, alisema wizara inaendelea na mazungumzo kupitia Ubalozi wa China ili kuleta nchini teknolojia ya majani yanayokua kwa haraka na yenye virutubisho bora ili kuondoa tatizo la ukosefu wa majani ya malisho kwa wafugaji.

RANCHI ZA TAIFA

Kuhusu ranchi za taifa, Ulega alisema serikali inakwenda kufanya uwekezaji wa kibiashara katika ranchi hizo ili ziwe kitovu cha uwekezaji wa biashara ya mifugo kwa kutoa nyama bora ya kutosha.

Alisema ranchi hizo zitaingia makubaliano na wafugaji kuwa na maeneo maalumu ya unenepeshaji mifugo.

"Ng'ombe wa asili jamii ya zebu anaponenepeshwa kila siku, kwa siku moja anaongezeka nusu kilo. Kama alikuwa na kilo 50 baada ya miezi minne atakuwa na kilo 110. Ukimchinja unapata nusu kwa nusu ambapo nyama itakuwa kilo 55 ambayo tayari ni soko.

"Ng'ombe wa kisasa anaponenepeshwa, kila siku ataongezeka kilo moja, mfano bora ni kama alikuwa na kilo 50 baada ya miezi mitatu, atakuwa na kilo 140, ukimchinja utapata kilo 70 ya nyama," alieleza.

Kwa sababu hiyo, alisema serikali imetilia mkazo upanuzi wa ng'ombe wa kisasa ili wafugaji wapate nyama nyingi.

KUKU

Kuhusu ufugaji wa kuku, alisema ni miongoni mwa vipaumbele vya wizara, ambapo kupitia dawati la kuku, utafiti wa kuhamarisha ufugaji kuku wa kienyeji umeanza kufanyika.

Alisema Taasisi ya Ufugaji Mifugo (TALIRI) wamechukua mbegu ya kuku wa asili aina ya kuchi ambayo inastahimili magonjwa.

UVUVI

Kwa upande wa sekta ya uvuvi, alisema mabonesho makubwa yanafanyika, ambapo kupitia bajeti ya mwaka huu, serikali inakwenda kununua meli nane za uvuvi kwa lengo la kumarisha uchumi wa bulu.

Alisema katika meli hizo nne zitatumika Tanzania bara katika uvuvi wa bahari kuu na maziwa, huku meli nne zitatumika upande wa Zanzibar.

"Tunataka tutumie muaji ya bahari na maziwa kuhakikisha mchango wa sekta ya uvuvi katika mainha ya Mkurunga unakuwa mkubwa. Kwa sasa wastani wa uvuvi unachangia asilimia 1.7 hadi 2.4 ya pato la taifa kwa mwaka na tunataka ufikie asilimia tano.

"Tutanunua meli hizo ili kumarisha uchumi wa bulu ambao bado haupokwenda, tunataka ufugaji wa samaki baharini na katika maziwa, tunataka tufuge majongoo bahari, kaa, tutengeneze viwanda na ndio maana tunafufua NYCO (Shirika la Uvuvi Tanzania) kwa ajili ya usimamizi wa meli na shughuli za uvuvi bahari," alisisitiza.

Alisema wizara ndani ya siku 100 za Rais Samia, imeboresha kanuni za uvuvi wa bahari kuu ambazo zilikuwa kikwazo ambapo sasa meli za uvuvi zimeanza kupi nchini na meli 20 za uvuvi wa bahari kuu zimeshachukuua leseni.

"Mambo ni mazuri katika uchumi wa bulu. Rais Samia ndiyo gwiji wa uchumi wa bulu. Kwa mara ya kwanza sheria ya uvuvi wa bahari kuu imewasilishwa Bunge la Wawakilishi, miaka yote tangu mwaka 2009 ilipowasilishwa bungeni haikuweza kuwasilishwa. Baraza la Wawakilishi ni kwa mara ya kwanza sheria imetibuka," Alisema.

Aliongeza kuwa: "Uchumi wa bulu ni pamoja na samaki, usafirishaji baharini, uchimbaji mafuta na gesi baharini na nder maana Rais Mama Samia anaungana mradi wa gesi ya LNG inayochimbwa baharini mkoani Lindi."

Scanned with CamScanner

MRADI

Ujenzi wa machinjio Vingunguti wasuasua

Mradi wa machinjio Vingunguti ulioanza Juni 2019 ulipaswa kukamilika Desemba 31 mwaka huo

Tatu Mohamed, Mwananchi
tmohamedi@Mwananchi.co.tz

Dar es Salaam. Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla ameliagiza Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kufanya kazi usiku na mchana ili Agosti mosi mwaka huu machinjio ya kisasa ya Vingunguti ianze kutumika.

Makalla alitoa kauli hiyo jana, alipotembelea machinjio hayo na kukuta bado haijaanza kutumika, huku Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam, Jumanne Shauri akisema ujenzi wake umekamilika kwa asilimia 96.

Ujenzi huo ulio chini ya NHC na mshauri mwelekezi akiwa M/Scons Africa Limited na FB Consultant, ulipaswa kukamilika Desemba 31, 2019.

Mradi huo ulioanza kutekelezwa Juni 2019, ulipaswa kukamilika baada ya miezi 18, lakini Rais wa Awamu ya Tano, hayati John Magufuli alifupisha mpaka miezi mitatu.

> **"Mkurugenzi amesema hela ipo na mfumo utafunguka, kwa hiyo niwaombe NHC jikusanyeni fanyeni kazi usiku na mchana ili tarehe moja hapa mambo yawe mazuri."**
> **Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla**

Septemba 16, 2019 Magufuli alifanya ziara ya kushtukiza katika machinjio hayo, akaeleza kutoridhishwa na mazingira ya eneo hilo na kasi ya ujenzi wa machinjio ya kisasa.

"Haiwezekani jengo la ghorofa moja tu lijengwe kwa miezi 18. Natoa maelekezo kuwa ndani ya miezi mitatu, yaani Oktoba hadi Desemba 31 mwaka huu, ujenzi uwe umekamilika," alisema Magufuli wakati huo.

Jana, Makalla alisema mradi unaenda kubadilisha uchumi na maisha ya watu, hivyo unatakiwa uanze kufanya kazi.

"Tumeambizana mchana kweupe, sasa hiyo Agosti mosi kazi ianze, mimi nitakuwepo hapa nikiangalia namna mnavyofanya hiyo kazi rasmi. Naomba iwe hivyo, sasa kazi zilizobaki zifanywe usiku na mchana," alisema.

Awali akizungumza, Shauri alisema mradi umefikia asilimia 96 na wamemlipa mkandarasi Sh9 bilioni.

Kaimu Mkurugenzi Uendeshaji Biashara NHC, Margaret Ezekiel alisema changamoto kubwa kwao ilikuwa ni fedha na walikuwa wanajitahidi kwa kutumia vyanzo vyao vya ndani.

"Wenzetu walikuwa wakitusaidia wanatupa kidogo kidogo, lakini hatujafikia mwisho bado tuna madeni kwao, hilo ndio limesuasua kidogo kufikia lengo la kuanza, lakini tumeshafanya tathmini ya awali, kwa ajili ya kuanza kutumika rasmi," alisema.

Scanned with CamScanner